

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa  
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## UFALME WA AINA MBILI —WA DUNIA NA WA MBINGUNI

*Kwa maana sisi, wenyiji [uraia, serikali] wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo. —Wafilipi 3:20*

Mashujaa wa imani ambao wanatajwa kwa mapana na mrefu katika kitabu cha Waebrania walitoka nchi mbali mbali, waliishi katika vizazi tofauti tofauti, walikuwa vifo vya aina tofauti tofauti, lakini wote walishiriki jambo moja: macho yao wote yalifunguliwa na mwanga wa kiroho ambao uliwafanya kukiri kwamba “walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi.” Na wakati wakitafuta nchi yao ya mbinguni lengo lao halikuwa kuwa makini au kusumbuka na mambo ya nyumba zao za humu duniani.

Watoto wa Mungu ambao wanaishi sasa hawana budi kuelewa kwamba wao ni watoto wa falme mbili. Ufalme mmoja ni wa hapa ulimwenguni na ufalme ule mwingine ni wa kiroho. Mtu huingia ufalme mmoja kwa kuzaliwa kimwili, na ule ufalme mwingine huingwa kwa mtu “kuzaliwa tena” kwa Roho wa Mungu (Yohana 3:3). Yesu Kristo ndiye mtawala wa ufalme wa pili, na Yeye alisema kwamba, “Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania” (Yohana 18:36). Ufalme wa Mungu uko ndani ya kila mtoto wa Mungu ambaye ameoshwa na damu yake Yesu (Luka 17:20-21). Huu sio ufalme wa kisiasa bali ni ufalme wa “haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu” (Warumi 14:17).

Watoto huwa raia wa nchi ambayo wamezaliwa. Ni jambo la kawaida na linalofaa kwa watoto kukua huku wakiwa na upendo wa kuitambua nchi zao. Uraia ni sehemu moja ya vile watu hujitambua na ni moja ya mambo yanayowezesha watu kujitambua kibinasi.

Lakini wakati mwingi watu huvutwa na roho ya utaifa wao na pia roho ya kujitolea kwa nchi yao. Watoto wao hufanya nadhara na uaminifu wao kwa nchi yao ya kidunia na hata kuilinda hivi kwamba wakati mwingine wanafikia hata kumwaga damu kwa ajili ya nchi zao. Wakati mwingi upendo huu kwa taifa huandamana na roho ya watu kujisikia kwamba wao ni bora kuliko watu wale wengine, jambo ambalo ni kinyume na Roho wa Mungu. Mara nyingi maslahi ya nchi moja huwa kinyume kabisa na maslahi ya nchi nyingine. Je, ni serikali gani au ni watu gani ambao wanafaa zaidi machoni pake Mungu? Je, ni taifa gani au ni malengo gani ambayo Kristo anaweza kutoa nadhiri au kujitoa kwayo? Ukweli ni kwamba katika Kristo “Hamna Myahudi au Myunani” (Wagalatia 3:28) kwa maana hata ingawa haya ni mataifa tofauti watu wote wa nchi hizo ni wa kiwango sawa katika Ufalme wa Mungu kuititia kwa mpango mkuu wa wokovu.

Hata ingawa watakatifu wa Mungu ni wananchi wa ufalme wa kidunia ambao ni nchi zao wao wameitwa kuwa wageni na watembezi duniani wakati wakitafuta mambo ya kiroho katika upendo na utumishi wao kwa Mungu. Watoto wa Mungu huwajibika kwa mwito wao wa juu zaidi na kwa jambo ambalo linahitaji uaminifu na kujitolea zaidi kuliko matakwa ya mataifa ya ulimwengu huu.

Sisi kama wananchi wa ufalme wa duniani na wa kiroho moja ya falme hizo ndiyo ambayo tutatilia umuhimu zaidi. Hata ingawa ni muhimu kwa watakatifu kuheshimu nchi zao na kuwa wananchi wenyi bidii ambao wanatii sheria za nchi zao, wao wanahitaji kujitolea mhanga na kufanya imani zao, tabia zao, maisha yao ya kila siku, ulingana na ufalme wa



*“Kwa kweli kufunga ni njia ya mtu kufungua akili na roho yake na kunyenyekoa mbele zake Mungu, jambo ambalo linamwezesha kushirikiana na Bwana kwa njia ya karibu zaidi katika mambo ya kiroho.”*

(Endelea katika Ukurasa 2)

Tahariri

Kujifunza Biblia:  
Mafundisho ya Biblia  
Kuhusu Msimamo wa Mkristo wa Kutopinga  
Mtu Mwovu

Mafundisho ya Biblia:  
Mafundisho ya Biblia  
Kuhusu Mkristo  
Kutopinga Mtu  
Mwovu

Maswali na Majibu

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

## Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

## Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

## Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

## Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,  
Efe. 2:1, 5-6

## Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

## Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

## Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,  
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

## Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

## Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,  
Kol. 1:18

## Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

## Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,  
Yn. 13:14-17

## Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

## Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,  
I Kor. 7:10-11

## Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

## Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,  
Mt. 25:31-46

## Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

## Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

## Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

kiroho badala ya ufalme wa kidunia. Wakati Yesu alipowaombea wanafunzi wake, katika Yohana 17:14-16 alisema kwa wazi kwamba wafuasi wake hata ingawa walikuwa wangali ulimwenguni, wao hawakuwa wa ulimwengu huu.

Wafuasi wa Yesu watakuwa na malengo na nia tofauti na zile ambazo zinaonekana katika falme za ulimwengu huu. Watakatifu wa Mungu wanahitaji kujikinga dhidi ya moyo yao na maisha yao kuambatana na nchi zao ili misimamo ya nchi zao isingongane na kanuni za kimsingi kuhusu upendo na unyenyekevu ambazo ndizo zinahitajika katika ufalme wa kiroho. Roho inayoleta misimamo mikali ya kisiasa au roho ya kimwili ya kuipinga serikali sio mambo ambayo yanalingana na Maandiko, hata iwe ni kwa sababu yoyote ile.

Hata ikiwa watakatifu walioko ulimwenguni kote ni wa tabaka, taifa, na lugha tofauti, umoja wao unapatikana ndani yake Yesu Kristo. Umoja huo kamwe hauhitaji kuvunjwa, na kamwe watakatifu hawastahili kuwa na ubishi wa mmoja kwa mwagine kwa ajili ya falme za kidunia. Watakatifu ni watu "walioitwa kutoka (duniani)" na hivyo wanahitaji kuishi kwa msingi huo.

Mtume Paulo akisema kuhusu vita vya kiroho katika 2 Timotheo 2:4 alisema, "Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeeye aliywandika awe askari." Watoto wa Mungu wanahitaji kuwa waangalifu ili wasifungwe na mambo ya ufalme huu wa kilimwengu. Siasa, utaifa, upinzani n.k. ni mambo ambayo yanaweza kuanza kutuongoza na kututawala na kumfanya mtu kwenda kinyume na kanuni zile kuu za milele za Bwana wetu Yesu Kristo.

## "Kuna msimamo ambao

Wakristo wanaweza

kuwa nao ambao

kupitia kwake tutaweza

kuishi katika amani na

kutambua kwamba hata

ingawa sisi tunaishi

katika falme za kidunia

utaifa wetu ulio mkuu na

wa kutambulika kabisa ni

ule wa ufalme wa kiroho."

wa Mungu wanastahili kuwa wenyewe shukrani kutokana na uhuru wa aina yoyote ambao umetolewa na serikali ambazo wao wanaishi ndani yake kama raia. Lakini shukrani hizo hazistahili kuandamana na ahadi za bure na hata kumfanya Mkristo kufanya nadhiri ambazo ni kinyume na uaminifu na kujitolea kwao kwa Mwana Kondoo wa Mungu. Sisi ni wasafiri na wageni nchini humu ambako tulimo, lakini baraka za utaifa wetu wa mbinguni ni kuu zaidi ya baraka zinazotolewa na serikali za kilimwengu.

Kuna msimamo ambao Wakristo wanaweza kuwa nao ambao kupitia kwake tutaweza kuishi katika amani na kutambua kwamba hata ingawa sisi tunaishi katika falme za kidunia utaifa wetu ulio mkuu na wa kutambulika kabisa ni ule ufalme wa kiroho. ■

Gazeti la Ukweli wa Injili ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwashimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tudembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la Ukweli wa Injili linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA  
editor@gospeltruth.org

# Tahariri



*Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.*

—1 Wakorintho 10:13

Somo la robo hii ya mwaka ni kuhusu swala la Mkristo kuwa na msimamo wa kutompinga mtu mwovu, au Mkristo kukataa kushiriki vita kwa sababu ya imani yake. Lakini kuna tofauti ya maana katika jambo hili, wakati mwingine likichukuliwa kuwa na maana ya mtu kuwa na mwelekeo wa kupinga vita vyote au mwelekeo wa kuipinga serikali, jambo ambalo liko kinyume na Mafundisho ya Agano Jipyä kuhusu mwelekeo huo wa Mkristo wa kutompinga mtu mwovu. Basi katika jarida hili maana ambayo imekusudiwa ni Mkristo kukataa kuwa mwanajeshi anayebeba silaha kwa sababu ya kidini.

Mafundisho haya kuhusu msimamo wa Mkristo kutompinga mtu mwovu yanapatikana katika Agano Jipyä na sio Agano la Kale. Lakini jambo hili halimaanishi kwamba mafundisho hayo hayana msingi kwa sababu mambo mengi yalibadilika kwa ukubwa wakati Kristo alipokuja. Lakini mafundisho hayo ya kutompinga mtu mwovu sio mafundisho ambayo watu dhaifu katika imani yao katika Kristo wanaweza kukubali. Kuna watu ambao wakisikia mafundisho haya wanawenza kucheka huku wakidhifikasi na kusema kwamba mwanaume wa kweli hujikinga wakati amekutana na adui. Lakini ukweli ni kwamba ni jambo ambalo linahitaji nguvu na uwezo zaidi kwa mtu kuwa na msimamo wa kupenda na kusamehe kuliko msimamo wa kupigana na makonde na silaha. Basi hata ingawa kanuni ya kutopinga mtu mwovu huangazia zaidi swala la kutoshiriki vitani; lakini kanuni hiyo pia inafundisha kuhusu njia bora zaidi ya kuishi, njia ambayo ina manufaa zaidi, njia ambayo kwa kuitumia tunaweza kuangusha na kubadilisha maadui zaidi ya vile ambavyo silaha hatari sana zinaweza kuwaangusha. Nguvu za msalaba (ambazo hazitumii silaha), na ambazo hupatikana kwa njia ya kunyenyeka, kamwe hazisalimu amri kutoptaka na woga wa kidunia. Badala yake nguvu hizo hukumbatia ulimwengu kwa upendo na wema.

Wakristo wataelewa kwa njia ambayo haifai mwito wa kumfuata Yesu huku wakiwa na msimamo wa kutompinga mtu mwovu kama hawataelewa vizuri kazi na wajibu wa kuweko na falme mbili tofauti. Hata ingawa Mungu ndiye ana haki ya kulipiza kisasi, Yeye hutumia serikali za kidunia kuleta hukumu duniani na kudumisha sheria na utaratibu mwema katikati mwa watu wasiomcha Mungu. Kwa kweli tunaweza kuheshimu na kufurahia serikali zetu na uhuru ambao zinatupatia, lakini kufanya hivyo sio lazima sisi tuwe na mwelekeo wa kujitolea kwa serikali hizo, mwelekeo ambao huenda ukawa kinyume na kujitolea kwetu na nadhiri yetu ambayo tunastahili kumpatia Mungu peke yake. Wakristo ni wagoni na wasafiri duniani. Sisi ni wapita njia ambao hatustahili kushikamana sana au kujishughulisha sana na maswala ya ulimwengu huu wa sasa. Siasa na jitihada za kuwaleta watu pamoja kwa ajili ya jambo fulani ambalo linawaletea watu hao shauku nyingi silo jambo ambalo linaonyesha roho wa Kristo. Huu ulimwengu ni nyumbani kwetu kwa muda tu, lakini tunastahili kutumia wakati mwingi na juhudhi zaidi kuijandaa kwa ajili ya makao yetu ya milele.

Katika mambo yote ambayo tutashiriki tunastahili kuijuliza swali kwamba, "Je, Yesu angeweza kushiriki jambo hili?" Tunahitaji kujibu swali hilo sio kulingana na maoni yetu ya kibinagsi bali kulingana na mfano ambao tulialiwa na Kristo. Kamwe hatumwoni Yesu akipigia debe harakati za uhuru wa kisiasa kwa njia ya kutumia vita au kwa kuandamana barabarani. Yesu hakuwaita Wakristo pamoja ili wafanye safari kuelekea mji wa Roma, wala hakuwaambia kusimama wima kujilinda dhidi ya wale ambao walikuwa wanawatesa. Lakini tunamwona Kristo ambaye alienda hatua zaidi kuliko alivyoamrisha, huku akiwafanya mema maadui zake na kuwapenda. Basi mfano ambao Kristo alitupatia hauambatani na matumizi ya mabavu, aidha ikiwa mtu ni mwananchi wa kawaada au kama mtu anaitumikia serikali. Sisi kama kanisa tunahitaji kutimiza wajibu wetu wa kibinagsi na wa pamoja, wajibu wa kueneza injili ya amani, na tuiachie serikali kufanya kazi yake bila kuingiliwa kwa mabavu.

Yohana D. Roth alitoa muhstasari wa jambo hili katika maandishi yake ya Kuamua Kwenda Kinyume na Vita (*Choosing Against War*), "Mwishowe, msimamo wa Mkristo wa kutoshiriki vita sio jambo la mabishano ambalo lazima mtu ashinde, na pia sio silaha ya mtu kufikia malengo mazuri ya kisiasa, na hata silo jambo la maadili mema ambayo kamwe hayatingisiki. Hili ni jambo hasa la mtu kumfuata Yesu kwa moyo wa kweli ambao umejitlelea mhanga, hata ikiwa safari hiyo itamfanya mtu huyo kufika msalabani."

Michael Smith  
Oktoba, 2018



Tutembelee

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

ili kuijandikisha na

kupata jarida

za mbele.

# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Mafundisho ya Biblia Kuhusu Msimamo wa Mkristo wa Kutopinga Mtu Mwovu

**Somo la Biblia:** Mmesikia kwamba imenenwa, jicho kwa jicho, na jino kwa jino; Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili.

—Mathayo 5:38-41



**Muhstasari:** Mafundisho na mfano ambao Yesu Kristo alitupatia unadhihirisha haja ya Mkristo kuishi maisha ya upendo na ya kutoppinga mtu mwovu. Yesu amewaita wanafunzi wake ili wafuate mfano wake wa kukabiliana na uovu na kutotendewa haki kwa kutumia silaha ya maombi, upendo, na kusameheana, badala ya silaha za kutumia nguvu na mabavu. Katika historia ya kanisa na hata sasa kanisa la Mungu limekuwa na msimamo wa kupinga Wakristo kushiriki katika jeshi.

**Maana: Kutoshindana na mtu mwovu**—Kanuni au mazoea ya Mkristo kutoshindana na mpinzani ambaye anatumia mabavu, au kutoipinga serikali kwa kutumia nguvu, hata ikiwa serikali hiyo inatumia ukatili na udhalimu.

**Kukataa kushiriki Vita**—Mtu kukataa kutumia silaha kama mwajeshi kwa ajili ya imani yake kuhusiana na maadili bora au kutokana na mafundisho anayoamini ya kidini.

### I. Unabii

- A. Yeremia 31:31 Agano Jipya (Waebrania 8:13)
- B. Mika 4:2-3 Watu wa Mungu hawatajifunza vita tena.

### II. Falme Mbili

- A. Wafilipi 3:20 Uraia wetu ni wa Mbinguni.
- B. Yohana 3:3 Mtu huingia Ufalme wa Mungu kupitia kwa kuzaliwa kwa njia ya kiroho.
- C. Luka 17:20-21 Ufalme wa Mungu ni ufalme wa kiroho (Warumi 14:17).
- D. Yohana 18:36 Ufalme wa Yesu sio wa ulimwengu huu.
- E. Yohana 17:14-16 Wanafunzi wa Kristo wako ulimwenguni lakini wao sio wa ulimwengu huu.
- F. Waebrania 11:13-16 Sisi ni wagoni na wasafiri duniani.
- G. Waefeso 2:19-20 Sisi tu raia pamoja na watakatifu wale wengine.

### III. Mafundisho ya Kristo—Sheria ya Upendo

- A. Mathayo 22:36-40 Upendo ndio amri kuu zaidi (Warumi 13:9-10).
- B. Mathayo 5:38-41 Usimpinge mtu mwovu (Luka 6:27-29).
- C. Mathayo 5:43-48 Miongozo ya jinsi mtu anahitaji kumpenda adui yake.

### IV. Vita vya Watakatifu

- A. Mathayo 26:51-52 Rudisha upanga wako.
- B. 2 Wakorintho 10:3-4 Silaha za watakatifu sio za kimwili.
- C. Waefeso 6:11-12 Mapigano yanahitaji kuwa ya kiroho, sio ya kimwili.

### V. Wajibu wa Serikali

- A. Danieli 2:21 Mungu huondoa na kuweka wafalme mamlakani (Zaburi 75:7).
- B. Danieli 4:17 Aliye Mkuu Zaidi ni mtawala katika falme za wanadamu.
- C. 1 Petro 2:13-14 Viongozi wa kidunia hupewa wajibu wao ili kuwaadhibu wenyewe kutenda maovu.
- D. Warumi 13:1-4 Lengo la kuweka serikali mamlakani ni kuleta hukumu kwa yule ambaye ametenda maovu (Yeremia 25:8-9).

### VI. Wajibu wa Watakatifu

- A. 1 Petro 2:21-24 Tumeitwa ili kufuata mfano wa Kristo wa kutoppinga mtu mwovu.
- B. 1 Petro 3:9 Wakristo hawastahili kulipiza uovu kwa uovu.
- C. 1 Petro 2:1-3 Kunyenyeka chini ya sheria na serikali za kidunia.
- D. 1 Timotheo 2:1-3 Waombeeni wale wote walioko kwenye mamlaka ili watakatifu waishi maisha yenye utulivu na amani.
- E. 2 Timotheo 2:3-4 Msijiingize sana kwa shughuli za kidunia.
- F. Warumi 12:14-21 Wabariki wanaokutesa. Usijilipizie kisasi.

### Tamati

*Kwa sababu ndio mliontiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake.*

—1 Petro 2:21


# Mafundisho ya Biblia Kuhusu Mkristo Kutopinga Mtu Mwovu

MWITO WA KRISTO KWAMBA TUISHI KWA SHERIA YA UPENDO

Yesu Kristo ndiye alianzisha mafundisho ya upendo ambayo yanasema kwamba watoto wa Mungu wanahitaji kustahimili kutotendewa haki bila kulipiza kisasi, na pia wasilipe maovu kwa maovu. Vita na umwagaji wa damu, mambo ambayo yalikuwa ya kawaida katika kipindi cha Agano la Kale sio mambo ambayo yanakubalika kwa watu wa Mungu amba wanaishi katika kipindi hiki cha neema ambacho sisi tunaishi ndani yake.

## Agano Jipyta

Hata ingawa vita na mafundisho ya kulipiza "jicho kwa jicho" yalikuwa mambo ya kimsingi na ya mazoea kwa taifa la (kihistoria) la Israeli kunalo agano jipyta ambalo lilitabiriwa katika agano hilo la kale. "Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipyta na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda" (Yeremia 31:31). Nabii Mika naye alitabiri kwamba kutakuja wakati ambapo watu wa Mungu "watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundi; taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe" (Mika 4:2-3). Unabii huu ultimia katika mpango wa wokovu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo.



"Ilikuwa  
wakati  
muhimu sana  
wakati Yesu,  
huku mauti  
ikimnukia,  
akimwambia  
Petro  
kurudisha  
upanga wake."

## Sheria ya Upendo

Katika Agano Jipyta watu wa Mungu wameitwa ili wafuate mafundisho na mfano wa Yesu Kristo. Kanuni la kimsingi la Kristo lilikuwa mafundisho kwamba mtu ampende Mungu kuliko kitu kingine chote na pia "Mpende jirani yako kama nafsi yako" (Mathayo 22:36-40). Watoto wa Mungu wanahitaji kuwa na upendo mkuu na kuwajali watu wale wengine wote, na kutaka watu wote wapate mema, hata wale amba wana tanda maovu. Ingawa wana wa Israeli walifuata sera za kivita hata kwa ajili ya kufuata mwongozo wa Mungu, Yesu alifundisha kwamba sisi tusishiriki vita na pia tusimpinge mtu mwovu. "Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa jino; Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili" (Mathayo 5:38-39). Andiko hili halikutoa mwongozo wa maisha ya mtu kibinafsi tu bali pia lilitoa mwongozo kwa watu wa taifa la Kiyahudi amba walishi chini ya himaya ya utawala wa kiimla wa serikali ya Rumi. Hata ingawa watu wengi walikuwa wakimtafuta Masihi ambaye angeshikanisha watu pamoja kufanya vita dhidi ya Warumi, Masihi halisi alitufundisha kwamba "tusishindane na mtu mwovu."

## Mfano wa Yesu

Je, ni kweli kwamba Yesu alimaanisha kwamba watu wake hawastahili kushiriki vita? Maneno yake hayakuwa tu ya ufasaha wa usemi au lugha ya kupendeza tu. Ukweli ni kwamba ilikuwa ni wakati mgumu sana wakati ambapo

Yesu huku akinukia mauti alimwambia Petro kurudisha upanga wake (Mathayo 26:52). Badala ya kukabiliana na uovu kwa kutumia mabavu na nguvu Yesu aliteseka bila kujibu kwa vitisho au matusi. Badala ya kutumia mbinu za vita na mabavu Yesu alimwombwa Baba yake kuwasamehe maadui zake. Basi Yeye akadhihirisha kuptitia kwa mfano wa maisha yake (na wanafunzi wake pia wakadhihirisha hayo) kwamba mateso na kuvumilia kutendewa vitendo visivyo vya haki na kujibu vitendo hivyo kwa upendo ni jambo ambalo ni bora zaidi kuliko Mkristo kulipiza kisasi au kujipigana kwa maslahi yake binafsi au hata kwa ajili ya taifa lake.

Wajibu wa watoto (wa kweli) wa Baba ni kuangusha mianzo yote ya vita na vurugu. "Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpati kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:43-45).

## Vita vya Kiroho

Mtume Paulo alizingumzia swala la vita vya kiroho na akasema wazi kwamba "Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;)" (2 Wakorintho 10:3-4). Maisha ya Mkristo yanahitaji kuwa ambayo yametolewa mhanga kutimiza kusudi la Yesu na yenye manufaa kwa ajili ya injili ya amani. Hata ingawa Wakristo wamo kwenye ubishi na vita katika maisha haya ubishi huo na vita hivyo ni vya kiroho na wala sio vya kimwili: "Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama" (Waefeso 6:11-12)

## Ushahidi wa Kihistoria

Kulingana na nakala za kihistoria na kwa kufuata mafundisho ya Kristo, Wakristo wa kwanza walikataa vita kabisa na pia wakakataa umwagaji wa damu. Wanahistoria wameashiria (hata ingawa hawajasema kwa njia ya moja kwa moja) kwamba kanuni ya kutoshindana na mtu mwovu imekuwa msimamo wa kanisa tangu mwanzo. Wakristo wa kwanza walikataa kutumika jeshini kwa sababu ya imani yao na kwa ajili ya utiifu wao kwa Kristo. Mwandishi Justin Martyr aliandika na kusema: "Sisi tumebadilisha vifaa

(Endelea katika Ukurasa 6)

vyetu vya vita vikawa majembe, mapanga yetu yakawa miundu; na mikuki yetu ikawa vifaa vya kulima." Nayo mafundisho ya kale ya kanisa (ambayo yamenakiliwa) yalikataza Wakristo kutumika jeshini.

## Serikali Za "Kikristo" Ndizo Zililetu Mchanganyiko



"Kuna tofauti kubwa kati ya majukumu ambayo mtoto wa Mungu ambaye anaishi katika neema kutokana na majukumu ambayo serikali imepewa na Mungu, majukumu ambayo hufanya kazi katika mambo ya kimwili."

wa Wakristo wa kutoipinga serikali, msimamo ambao ndio ulikuwa na Wakristo wa kwanza. Wale ambao walikuwa viongozi wa msimamo huu mpya ilikuwa ni viongozi wa kijeshi, ambao sasa hata walifanya vita kwa jina la kuwa Wakristo.

## Mgawanyiko Kati ya Mambo ya Kidunia na ya Kiroho

Hata sasa Wakristo wengi wameingiliana na mambo ya kidunia katika msimamo wao kuhusu swala hili. Lakini Msimamo wa mtoto wa Mungu kuhusiana na swala la kutompinga mtu mwovu hauhitaji kuwa umetokana na historia, bali unahitaji kuwa umetokana na mafundisho rahisi ya Kristo. Ni jambo la kimsingi mtu kutambua kwamba kuna falme mbili—ufalme mmoja ukiwa wa mpito na mwingine ukiwa wa kiroho. Ufalme wa Mungu sio "wa ulimwengu huu" (Yohana 18:36) na hata ingawa Wakristo wako ulimwenguni wao sio wa ulimwengu huu (Yohana 17:14-16). Kama wagoni na wapita njia watakatifu wa Ufalme wa Mungu wanastahili kuepuka vita vya kisasa vya kupigania mambo ya mpito na ambavyo hufanya kwa jina la taifa, kwa sababu vita hivyo huwa kinyume na matakwa ya uraia wa ufalme wa kiroho. Kuna tofauti kubwa kati ya majukumu ambayo mtoto wa Mungu ambaye anaishi katika neema yakilinganishwa na majukumu ambayo serikali

imepewa na Mungu, majukumu ambayo hufanya kwa njia ya kimwili. Wakati mwingi majukumu hayo mawili kamwe hayaingiliani.

## Mungu Ndiye Ameweeka Serikali Mamlakani

Kitabuli cha Danieli kinatufunza kwamba Mungu ndiye "huuzulu wafalme na kuwamilikisha wafalme" (2:21). "Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, tena humtawaza juu yake aliye mnyonge" (4:17). Hata ingawa serikali hazina uwezo wa kuleta matangamano na amani kamili kwa kutumia sheria kutokana na sababu kwamba wanadamu wengi wamekataa neema ya Mungu, serikali huweza kusaidia kuzuia virugu kwa kutumia mbinu za kimwili. Hii ndiyo sababu Mungu ametoa mweke kwa wafalme na watawala kuadhibu watu wenye kutenda maovu (1 Petro 2:13-14). Basi sio kazi ya watakatifu ambao wanaishi chini ya neema na upendo kuwapatia adhabu wale watu ambao wanatumia mabavu, au wale ambao ni wezi hatari, au hata mataifa ambayo huualetea wananchi wao madhara. Serikali za kidunia zimeitwa "watumishi wa Mungu" ambao wamekekwa mamlakani na Mungu ili wawe - "amlipizaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu" (Warumi 13:1-4).

## Wito Ambao Mkristo Amepata

Huduma ya kanisa ni kuendeleza umisheni wa Kristo duniani. Huduma ya Kristo haikuwa ya kumwadhibu mtenda maovu bali ilikuwa kuleta ujumbe wa wokovu na upendo kwa ulimwengu ulioanguka. Hata ingawa Wakristo ni raia wa ulimwengu huu mwito wao ni kuishi kulingana na mwito wa juu zaidi. Biblia imetaja wazi wazi kuhusu wajibu na majukumu ya mtoto wa Mungu. "Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana" (1 Petro 2:13). Wakristo wanastahili kutii sheria za nchi yao mradi iwe kwamba sheria hizo hazihitilafiani na sheria ya Mungu. Wakristo wanastahili kuomba na kufanya sala "kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu" (1 Timotheo 2:1-3). Lengo letu ni kuishi maisha yenye utulivu na amani; na kama wanajeshi wa msalaba Wakristo hatustahili kuingiliana sana na mambo ya maisha sasa (2 Timotheo 2:3-4).

Wakati huu ambapo vita vinaendelea duniani na mataifa mengine yanapata nguvu na mengine kuanguka watakatifu wa Mungu wanastahili kuendelea kufuata nyayo zake Kristo (1 Petro 2:21-24)—nyayo za kutolipisha "baya kwa baya" (1 Petro 3:9), kusimama wima kuwapenda wenzao, kufanya mema kwa maadui zao (wa kibinagsi na wa kitaifa), kuwabariki watesi wao, na kushinda uovu kwa kutenda wema (Warumi 12:14-21).

Msimamo wa watakatifu wa kukataa kutumika jeshini ni jambo ambalo msingi wake ni mafundisho na mfano wa Mfalme wa Amani. Ni kweli kwamba msimamo wa kutompinga mtu mwovu ni jambo ambalo ulimwengu hautaelewa, na ni jambo ambalo litaleta mateso, na hata wakati mwingine litaleta mauti; lakini hayo yote ni matokeo ya kufuata njia nyembamba, njia ambayo humwongoza mtu hadi katika uzima wa milele. ■

# Maswali na Majibu

## Je, ni jambo ambalo halifai Wakristo kutumia nguvu ili kujilinda?

Swali hili huzua hisia na ubishi mwingu. Ni jambo muhimu kukumbuka kwamba Wakristo (kwa makosa) walizua dhana ya "vita vya haki" ili wapatanishe vita na mafundisho ya kutompinga mtu mwovu. Dhana hiyo inaweza kutumika katika maisha yetu ya kibinagsi. Yesu mwenyewe hakujikinga wakati akichapwa na kusulubishwa. Nao mitume wa Kristo na maelfu ya watu wengine ambao waliuawa kwa ajili ya dini hawakulipiza kisasi au kufanya vita ili kujilinda wakati wakiuawa kwa njia isiyo ya haki. Ni jambo ambalo si la akili timamu mtu kukosa kujilinda wakati yumo hatarini. Basi ni kwa njia ya neema tu na ya kiungu na ya kutokana na uwezo wa Mungu ndipo mtu huweza kukabiliana na hali kama hiyo kwa kutumia nguvu zaidi ambazo amepewa na Mungu, nguvu za upendo na msamaha.

Kuna wakati ambapo halaiki ya watu walijaribu kumshika Yesu ili wamuue. Lakini Yeye aliweza kuwahepa na kutoroka mbali nao kwa zaidi ya mara moja. Basi tendo la Mkristo la kumhepa mtu mwenye kuleta madhara sio kitu moja na yeze kutumia nguvu za kimwili ili kujilinda. Lakini kuna hali nyingi ambazo zinaweza kuelezewa kwamba ziko kinyume na ukweli huu. Mimi mwenyewe ninakubali kwamba siwezi kuwaambia watoto wasitumie nguvu za kimwili ili kuhepa na kumtoroka mtu ambaye amewateka nyara. Mungu ameahidi kwamba hatatuleta majoribu ambayo ni zaidi ya yale ambayo tunaweza kustahimili, basi ninaamini kwamba tukijipata katika hali mbaya zaidi kutakuwa na neema kubwa zaidi na hekima kubwa zaidi kutoka kwake Mungu ambayo itatuwezesha kuendelea kuishi maisha ambayo yanalingana na mafundisho yake Kristo.

## Je, ni vipi Mkristo anaweza kuunga mkono utawala wa sheria na kazi ya wanajeshi?

Kama Wakristo wazuri silo jambo la kinafiki sisi kufurahia kazi na wajibu wa serikali wa kuhakikisha kwamba sheria inafuatwa, na pia kufurahia kazi ya wanajeshi, hata ingawa sisi wenyewe hatushiriki vitani ambako inatubidi tuwaue watu. Kama hakungalikuwa na wadumishaji wa amani wa kitaifa na hata wa kilimwengu kungalikuwa na vurugu ulimwenguni kote na uhuru tulio nao ungekuwa hafifu kabisa. Sisi tuko na uhuru ambao tuko nao kwa sababu ya kujitolea kwa watu ambao kila siku wanahatarisha maisha yao kwa ajili ya manufaa yetu. Ukweli ni kwamba kuna mambo ambayo tunaweza kufanya ili kuunga mkono walinda usalama, mambo mengine yakiwa vitendo vya kiroho vya kuwanufaisha walinda usalama. Ni jambo muhimu kwetu kukumbuka kwamba sisi ni raia wa nchi mbili. Huduma yetu ya kwanza kabisa na mwongozo wetu maishani unahitaji kuwa kwa ajili ya manufaa ya mambo ya kiroho, lakini hivyo si kusema kwamba hatuwezi kufurahia kazi ya watu wale wengine.

Pia ni jambo muhimu kwa Wakristo kutotilia umuhimu mkubwa kazi ya serikali, hata ingawa kazi ambazo serikali hizo hufanya ni muhimu kwa ajili ya manufaa ya watu wale ambao hawaishi kwenye neema. Basi si jambo bora sisi kupigia debe kwa watoto wetu kufanya kazi katika huduma za kidunia ambazo hazilingani na maisha yetu ya Kikristo.

## JE, TUSEME NINI KUHUSU WATU WANAOKATAA KUTUMIKA JESHINI KWA SABAU YA DHAMIRI ZAO?

*Kumtii Mungu Badala ya Kumtii Mwanadamu*

Kuna watu ambao hukataa kutumika jeshini au kukataa kubeba silaha kutokana na msimamo au maadili yanayoongoza maisha yao, au kutokana na msimamo wao wa kidini. Katika historia kuna rekodi ya watu wengi ambao walikumbatia msimamo huo wa kutoshiriki jeshini, na kutokana na hayo wakafungwa jela au hata kuuawa wakati ambapo imani yao iligongana na msimamo wa serikali zao.

Lakini baadhi ya watu hawa ambao walikataa ktutumika jeshini kwa ajili ya dhamiri zao mara nyingi walikuwa tayari kufanya huduma jeshini ambazo hazikuhusisha matumizi ya silaha, lakini kuna wengine wao ambao walipinga utumishi wa aina yote jeshini. Katika siku za hivi karibuni baadhi ya nchi zimetoa kibali na kuruhusu watu wanaokataa kushiriki jeshini kwa sababu ya dhamiri na dini zao kuweza kufanya hivyo. Baadhi ya nchi hizo zimetoa njia mbadala ya watu hawa kutumika, badala ya wao kubeba silaha, huduma kama ile ya wananchi wa kawaida, badala ya wao kulazimishwa kutumika jeshini.

Wakristo wanahitaji kufanya juu chini ili kufanya mambo yote wanayotenda yalingane na sheria ambazo serikali zao zimeunda ili wawewe kuwa raia wanaoleta manufaa kwa kufuata sheria. Lakini wakati jambo fulani linapohitilafiana na roho yake Kristo basi Mkristo hana budi kwa unyenyekevu mkubwa kuitii sheria ya Mungu badala ya kutii sheria ya mwanadamu. ■





**JE, WAJUA?**

## ***Usiue. —Kutoka 20:13***

Baadhi ya tafsiri za biblia hutumia neno “usiue” katika andiko hili lakini ni bora zaidi ikiwa andiko hili lingetafsiriwa “usipange kumuua mtu.” Jambo hili ni tendo la mtu kupanga kumwua mwenzake kinyume na sheria, kwa kusudia, na kwa nia mbaya.

Tunaona katika maandiko kwamba mara tu amri hiyo ilipotolewa Mungu alishaagiza Walawi kuchukua silaha zao na kuwaa watu amba walikuwa wameanza kuabudu miungu isio ya kweli. Basi kwa kutoa amri hiyo Mungu hakuwa akienda kinyume na sheria ambayo alikuwa ametoa hapo tu mbeleni kwa Musa, kwa maana mauaji hayo ambayo aliamuru Walawi walikuwa wafanye yalikuwa ni ya kulingana na haki.

Hata ingawa Biblia imeweka umuhimu na gharama kubwa kwa maisha ya mwanadamu, amri hiyo ambayo inapatikana hapa sio msingi wa mafundisho ya Biblia kuhusiana na msimamo wa Mkristo wa kutompinga mtu mwovu. ■




## **TAMASHA KWA DUNIA**

*Maana nadhani ya kuwa Mungu ametutoa sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauawee; kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu. Sisi tu wapumbavu kwa ajili ya Kristo . . . —1 Wakorintho 4:9-13*

Katika 1 Wakorintho 4:9-13 Mtume Paulo amechora mchoro kuhusu majoribu na mateso ya mitume. Mchoro huo ni wenye kuwapa nguvu na changamoto wahudumu wa injili ambao tayari wametoa maisha yao kwa ajili ya Injili.

Katika andiko hilo Mtume Paulo anaguzia mazoea ya Warumi kufanya tamasha katika uwanja wa michezo ambao ulikuwa na jukwaa na ambako watu waliojihami silaha wangepigana na wanyama mwitu. Kama watu hao wangeshinda wanyama hao wa mwitu mara moja wao wangenyang’anywa silaha na kuachwa bila kitu cha kujilinda dhidi ya wanyama na hata wanadamu wenzao. Na kama wangefaulu kuhepa na kutoroka mwishowe wangelazimishwa kukabiliana na mvamizi wa aina nyingine ambaye bila shaka angewaletea mauti. Basi kama ilivyokuwa kwa mtume Paulo wahudumu wa injili wanaweza kupatwa na majoribu mengi, masumbufo, mashtaka yasiyo ya kweli, ufukara, na hata mateso maishani mwao kwa sababu ya jina lake Kristo; lakini ni heshima kubwa kwa mwanadamu kuhesabiwa kwamba anafaa kuteseka kwa ajili ya Kristo.



### **UTAKATIFU KWA BWANA**

Anwani

The Gospel Truth  
P. O. Box 2042  
Nixa, MO 65714  
USA

Email:  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

Watu wa Mungu wakati mwingu huwa ni “tamasha kwa ulimwengu.” Tamasha hii huashiria kile ambacho kilifanyika katika uwanja huo kwenye jukwaa ambako wapinganaji walifanya mapigano. Kwenye uwanja huo kulikuwa na viti ambavyo vilizunguka jukwaa hilo ambako maelfu ya watu wangeweza kukaa kushuhudia mauti ya uhakika ambayo iliabidi watumbuizaji hao au mhalifu wa kawaida ambaye alishahukumiwa kifo kupatana nacho. Watakatifu wa Mungu wamezungukwa na ulimwengu na wakati mwingu wenye dhambi duniani huwachekelea Wakristo wanapowatazama kwa macho ya kidunia. Kanuni ambazo zinaongoza moyo na nafsi ya mtoto wa Mungu ni tofauti kabisa na zinazoongoza watu wa ulimwengu. Kusema kweli ulimwengu hauelewi jambo hili na mara nyingi ulimwengu huwachekelea na kuwatenga watoto wa Mungu kwa sababu watoto wa Mungu huonekana na hutenda mambo tofauti na ulimwengu. Watoto wa Mungu hupenda watu na kuwasamehe badala ya kujilipiza kisasi au kupigana. Wao huhubiri unyenyekevu, upendo, na umoja badala ya kuhubiri haja ya wanadamu kuokoa nafsi zao kwa njia ya kimwili au kwa kujitakia makuu. Basi si jambo la kustajabisha kwamba watakatifu wa Mungu huwa kama tamasha la kutazamwa na walimwengu.

Adui yetu hufanya juu chini ili kufanya wahudumu wa injili amba wako kwenye mstari wa mbele wafe moyo na kuacha huduma wanayofanya. Lakini badala ya kufa moyo na kujihishi kushushwa moyo kutoptana na mateso ya uhakika ambayo tunapata mhudumu wa injili ya Mungu anahitaji kujipa moyo. Hatuna haja ya kuona aibu kwa sababu ya kusimama wima katika Neno la Mungu na kwa sababu ya kutangaza ujumbe wenye kuleta uhai, ujumbe wa wokovu na utakatifu. Kama vile ambavyo watu wengine wameteseka kwa ajili ya Kristo, sisi nasi hatuna budi kuteseka. Basi wewe mtoto wa Mungu uendelee kuwa mwaminifu, kwa maana sisi ni wafalme na makuhani katika ufalme wa Bwana wetu. ■